



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA



Kumb. Na. DED/IRA/E. 20/1/95

13 Septemba 2024.

## TANGAZO

Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba anawatangazia Watumishi wa Umma wote nafasi za kazi kwa ajili ya shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe **27 Novemba, 2024**.

1. **Nafasi zinazotangazwa:-**

- (a) Msimamizi wa Kituo
- (b) Afisa Mwandikishaji wa Wapiga kura

2. **Sifa zinazotakiwa**

- (a) Aslwe na dhamana au Uongozi katika Chama chochote cha siasa
- (b) Awe ni Mtumishi katika Utumishi wa Umma (Public Service).
- (c) Awe Mwadilifu.

3. **Namna ya kuandika barua**

- Barua zote ziandikwe kwa mkono
- Barua iandikwe majina kamili yanayotumika katika Utumishi
- Barua itaje nafasi ya kazi unayoomba.
- Barua itaje cheo katika Utumishi wa Umma
- Barua itaje kituo cha kazi
- Barua iwe na anuani kamili ikiwa na namba ya simu inayopatikana wakati wote
- Barua iambatishwe na maelezo binafsi (CV)
- Barua ziwasllishwe kwa mkono masijala ya wazi ya Mkurugenzi Mtendaji.
- Mwombaji atatakiwa kusaini daftari la kupokelea barua za maombi.
- Barua iandikwe kwa:

Msimamizi wa Uchaguzi,  
Halmashauri ya Wilaya  
ya Iramba, S.L.P 155,  
**IRAMBA.**

4. **Mwisho**

Mwisho wa kupokea barua hizo ni tarehe 20 Septemba, 2024 siku ya Ijumaa saa 9.30 Alasiri.

Wakatabahu,

Magreth C. Segu,

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**  
**JIMBO LA IRAMBA MAGHARIBI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA**

## MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

Ukusa wa 1 Kali ya Kurasa 1